Digital Enquirer Kit

ya Vijana

# Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali (DEK) Ya Vijana

## Kitabu cha Mwongozo kwa ajili ya Wakufunzi

Wahisani

Co-funded by the European Union

german cooperation DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT

Implemented by giz

Watekelezi na Wasimamizi

atingi learn.connect.act.

#smart development fund

SEITEN STARK

# Yaliyomo


**Utangulizi** .......................................................Fehler! Textmarke nicht definiert.

Kwanini Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali (Digital Enquirer Kit) ya Vijana?................ 3

Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali (Digital Enquirer Kit) ya Vijana ni nini, na hutumika wapi?........................................................................................................ 3

Ninapata wapi Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth)? .................. 4

Kwanini kuwepo mwongozo huu kwa mkufunzi, na jukumu langu ni lipi kama mkufunzi wa Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth)?..................... 4

**Sura ya 1: Kutazama kwa ukaribu zaidi Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth) .......................................................................................6**

Muundo wa Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth) ukoje? ............ 6

Ninahitaji teknolojia gani ili kuweza kutumia Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth)?.................................................................................... 7


Je, ninaweza kutumia Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth) bila mtandao wa intaneti? ........................................................................... 7

**Sura ya 2: Mafunzo yaliyopo kwenye Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK-Youth) yanahusu nini, na ninaweza kupitia changamoto gani pindi ninapofanyia kazi Nyenzo hii ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK-Youth)?........8**

Unawezaje kutumia Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth) katika kuunga mkono mafunzo ya vijana? ........................................................ 17

Ninaweza kutumia njia gani kupanua maudhui ya Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth) kwa kina zaidi? .................................................. 18

**Sura ya 3: Tafakari juu ya unyeti wa masuala ya mgogoro, maumivu ya matukio yaliyopita, na mwingiliano wa upendeleo na ubaguzi .........................................19**

# Utangulizi

## Kwanini Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (Digital Enquirer Kit Youth)?

Udigitali unaenea kwa kasi ulimwenguni kote. Sambamba na faida zake, kama vile urahisishwaji wa mawasiliano na mitandao, changamoto na hatari mpya huibuka. Hatari hizi huathiri watumizi wote, hasa walio na umri mdogo. Kote ulimwenguni, vijana wamekuwa miongoni mwa kundi kubwa zaidi zitumiazo programu-tumizi zinazopatikana kwenye vifaa vya simu. Matumizi ya intaneti na simu janja yamekuwa na ushawishi mkubwa katika namna vijana wanavyojitambua wenyewe. Katika mitandao ya kijamii, vijana hukumbana na picha na jumbe zenye taarifa ambazo mara nyingi, huwa hazijahakikishwa. Ni ngumu kutofautisha maoni ya ripoti na uvumi na kweli zilizopo, jambo hili laweza kusababisha tafrani. Aidha, maudhui ya uhasama yanaweza kusambazwa upesi na kutumika kuchochea uhasama wa kidigitali, kama vile matamko ya chuki ama uonevu ufanyikao kwenye mitandao ya kijamii. Kwa urahisi, vijana wanaweza kuhisi kulemewa na kutokuwa salama kutokana na kiasi cha taarifa kilichopo.

## Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (Digital Enquirer Kit Youth) ni nini, na hutumika wapi?

Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth) ni programu ya mafunzo ya mtandaoni, iliyo rafiki kwa watoto na vijana, ihusuyo masuala ya usalama wa kidigitali na taarifa potofu, inayoweza kutumiwa na wanafunzi wote walio na umri unaozidi miaka 10. Kile tu unachohitaji ni kifaa cha simu na muunganisho wa intaneti.

Ikiwa na mada elekevu, shughuli zilizo rahisi kufanya, na vipindi vya tafakari, Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth) huwasaidia vijana katika kukabiliana na changamoto zilizotajwa hapo juu. Huwahimiza wanafunzi kufikiri juu ya athari ya uenezi wa kasi wa taarifa za uongo na huwasaidia kujifunza namna ya kuhakiki maudhui wanayoyaona mtandaoni. Pia, Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth) huwawezesha wanafunzi kuabiri hatari za intaneti na huwafundisha namna ya kushughulikia athari zake zilizoshamiri katika maisha yao ya mtandaoni ya kila siku. Kwa kujenga uwezo wa vijana wa kutumia intaneti kwa usalama katika namna yenye msingi wa thamani, Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth) huunga mkono matengenezo ya jamii za kistaarabu za kidigitali.

Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth) imeundwa kwa kuzingatia mkakati wa kielimu ulio kama daraja na zana iliyojizatiti katika kudumisha amani. Huwahimiza vijana kupanua ufahamu na ujuzi wao, na kushiriki katika maudhui ya mtandaoni katika namna ya kujitafakari na izingatiayo thamani. Hili ni pamoja na kuhoji kwa umakini vitendo na tabia zao wenyewe walizonazo mtandaoni.

Kama programu ya mtandaoni, Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth) hufaa kutumika katika:

- mafunzo ya kujitegemea yaliyopo mtandaoni, popote pale
- kitengo cha habari mashuleni
- shughuli zifanywazo na kundi za vijana au taasisi

Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth) hufaa pia kwa matumizi ya uwezeshaji kwani huweza kujumuishwa katika utoaji wa elimu ya ana kwa ana, nje ya mtandao, rasmi au hata isiyo rasmi.

## Ninapata wapi Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth)?

Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth) hupatikana bure mtandaoni, katika lugha saba.

## Kwanini kuwepo mwongozo huu kwa wakufunzi, na jukumu langu kama mkufunzi wa Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth) ni lipi?

Mwongozo huu umedhumuniwa kwa ajili yako kama mkufunzi na hukupatia maelezo ya jumla kuhusu:

- muundo, maudhui, na malengo ya masomo manane yaliyopo kwenye Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth)
- mawazo juu ya namna ya kuunga mkono mafunzo ya vijana

Kwa kutoa msaada wa kielimu kwa ajili ya Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth), unawatengeneza watumizi walio vijana fursa ya kuimarisha na kutafakari ufahamu na ujuzi waliojifunza wao kama wao.


Lengo la ziada la mwongozo huu ni kukuhimiza kuchunguza kwa umakini maudhui haya na jukumu ulilonalo.

Kama mkufunzi, kazi yako si kuongoza kipindi tu. Hauna budi kuenenda pia kama mfano wa kuigwa. Unaelewa mazingira ya kijeografia, ya kijamii na ya kisiasa yanayokuzunguka. Kwa kusema ‘mazingira’ tunamaanisha madhari mahsusi ya mafunzo, pamoja na jamii au muktadha mpana zaidi wa kikanda ambao katika huo, shule au kituo cha vijana hupatikana.

Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth) ilitengenezwa ili kutumika kote ulimwenguni, kwani haijaundwa kufaa hali ya kanda au muktdha mutktadha fulani mahsusi pekee. Hivyo basi, tunakuhimiza kufanya maudhui haya kuendana na jamii uliyopo na kufaa mahitaji ya hadhira uliyonayo, lakini pia, kuilinda katika namna ambayo utaweza kuitumia kwa uasilia. Vivyo hivyo ndivyo ilivyo na katika mwongozo huu.

Ujanibishaji na uasili wa hali iliyopo ni muhimu kwani kila mazingira na hadhira lengwa huwa na upekee wake. Kwa mujibu wa uzoefu wetu kama wakufunzi, vipengele vitatu miongoni mwa vilivyo muhimu zaidi ni unyeti wa masuala ya migogoro, maumivu ya matukio ya nyuma, na mwingiliano wa upendeleo na ubaguzi. Ndani ya Sura ya 3, mwongozo huu utakusukuma

kujizatiti kwenye vipengele hivi kabla ya kuanza kuifanyia kazi Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth).



# Sura ya 1: Kuitazama kwa ukaribu zaidi Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth)

## Muundo wa Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth) ukoje?

Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK-Youth) inajumuisha masomo manane shirikishi, yaliyogawanywa katika sura fupi-fupi: Mhusika 'Kobe' anaungana na watumizi wa nyenzo hii katika safari yao ya kujifunza:

**Maelezo ya Jumla kuhusu vipengele na masomo:**

| Mada | Somo namba° | Kichwa cha somo |
|---|---|---|
| Wewe na ulimwengu wa kidigitali – Tuzame katika bahari hii pana kwa pamoja | Somo la 1 | Je, wewe ni Mdadisi wa Kidigitali (Digital Enquirer) makini? |
| | Somo la 2 | Unawezaje kutumia intaneti kwa usalama? |
| Wewe na taarifa za uongo – Jifunze kilichopo huko nje | Somo la 3 | Taarifa ya uongo ni nini? Kwanini na kwa jinsi gani inaweza kuenea? |
| | Somo la 4 | Unatambuaje taarifa ya uongo? |
| | Somo la 5 | Taarifa ya uongo inawezaje kukuathiri na unaweza kufanya nini kuhusu hilo? |
| Wewe na marafiki zako – Fahamu namna ya kufurahi na kuwa salama huko nje | Somo la 6 | Hatari za ulimwengu wa kidigitali ni zipi? |
| | Somo la 7 | Unawezaje kujilinda na kuwalinda wengine dhidi ya ukatili wa kidigitali? |
| U tayari sasa kuyakabili mawimbi ya bahari kuu | Somo la 8 | U tayari sasa kuyakabili mawimbi ya bahari kuu! |

Kila somo ni zana inayojitosheleza, inayojumuisha muhtasari mfupi wa mada muhimu zaidi. Ingawa tunapendekeza kwamba ufuate mtiririko uliopo katika masomo haya, hili si lazima kwani maudhui haya bado yanaweza kueleweka hata bila ya kufanya hivyo.

Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK-Youth) haitumii vidakuzi. Hivyo, watumizi hawataweza kuhifadhi rekodi ya maendeleo waliyofikia katika mada husika. Hata hivyo, wataweza kuteua moja kwa moja somo lolote watakalolitaka.

Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK-Youth) inatolewa sambamba na 'Kituo cha Rasilimali', ambacho hutoa fafanuzi juu ya baadhi ya maudhui yaliyopo kwenye nyenzo hii. Tafadhali zingatia kwamba, baadhi ya viungo vilivyoorodheshwa ndani ya Kituo cha Rasilimali hutumia vidakuzi. Pengine, unaweza kuona vema kuitazama mada mahsusi ya vidakuzi inayoweza kukutaka kutoa idhini yako ndani ya kipindi husika. Unaweza kupata taarifa zaidi kuhusu vidakuzi ndani ya Kituo cha Rasilimali za Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK-Youth) Kituo cha Rasilimali | Digital Enquirer Kit Youth (atingi.org).

## Ninahitaji teknolojia gani ili kuweza kutumia Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK-Youth)?

Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK-Youth) imeundwa kuweza kutumika katika vifaa vya simu, lakini pia katika vifaa vingine kama vile kompyuta za mezani. Kile tu kinachohitajika ni muunganisho mzuri wa intaneti. Muundo wa Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK-Youth) huruhusu utendakazi hata pale panapokuwepo kiwango hafifu cha masafa ya mtandao. Matumizi ya data hayaathiriwi na madoido ya sauti zilizopo kwenye Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK-Youth). Mtumizi anaweza kuwasha au kuzima sauti hizi kupitia mipangilio ya utendakazi wa kifaa husika.

## Je, ninaweza kutumia Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK-Youth) bila mtandao wa intaneti?

Kwa sasa, haiwezekani kupakua Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK-Youth). Ikiwa utapenda kutumia sehemu yoyote ya maudhui yake bila ya kuwa mtandao wa intaneti, tunapendekeza kwamba unakili na kubandika sehemu hizo husika, nasa picha za skrini, na zichapishe au tengeneza matini.



# Sura ya 2: Mafunzo yaliyopo kwenye Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK-Youth) yanahusu nini, na ninaweza kupitia changamoto gani pindi ninapofanyia kazi Nyenzo hii ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth)?


## Somo la 1: Je, wewe ni Mdadisi wa Kidigitali (Digital Enquirer) makini?

### Malengo ya Mafunzo

| | |
|---|---|
| Wanafunzi watajifunza kuhusu kazi za Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK-Youth). | Wanafunzi watatambulishwa katika mada za Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK-Youth) (kama vile taarifa za uongo, usalama wa kidigitali, na hatari zilizopo kwenye intaneti). |

### Maswali ya tafakari yanayoweza kutumika

- ? Unatumia muda kiasi gani mtandaoni kila siku?
- ? Unafanya nini ukiwa mtandaoni? Unatumia tovuti, programu-tumizi au jukwaa zipi za mitandao ya kijamii?
- ? Ni jumbe, picha, au video gani umezishirikisha hivi karibuni mtandaoni?
- ? Je, umewahi kuhisi wasiwasi au kuhangaika kihisia baada ya kushirikisha kitu mtandaoni?
- ? Unapenda au hupendi nini kuhusu ushirikishaji wa vitu mtandaoni?



# Somo la 2: Unawezaje kutumia Intaneti kwa usalama?

## Malengo ya Mafunzo

| | |
|---|---|
| Wanafunzi watatambua namna ya kulinda data zao binafsi mtandaoni na wataweza kutathmini kwa umakini namna mbalimbali za kulinda vifaa vyao. | Wanafunzi wataasili vipengele muhimu vya namna ya kuabiri katika intaneti kwa usalama. |

## Maswali ya tafakari yanayoweza kutumika

- ? Unavilindaje vifaa vyako na kwa nini unavilinda kwa namna hiyo?
- ? Unashirikisha taarifa zipi binafsi kwenye mitandao ya kijamii?
- ? Kati ya mtandaoni na nje ya mtandao, ni wapi ni rahisi zaidi kulinda taarifa zako binafsi kama vile tarehe ya kuzaliwa, anuani yako, au nambari yako ya simu? Kwanini?
- ? Unafikiri ni kwanini watengeneza tovuti hutaka kufahamu mwenendo wako mtandaoni? Kwanini hili linaweza kuwa tatizo?

## Changamoto zinazoweza kuibuka

**Ulinzi wa Data:** Katika Somo la 2, baadhi ya washiriki wanaweza kudhani kuwa ulinzi wa data binafsi si jambo muhimu. Kwa mfano, wanaweza kudai kwamba, ulinzi wa data ni jambo linalohitaji kutumia nguvu nyingi mno. Mara nyingi, hasa ya vijana, huwa ni ngumu kuelewa kwanini ulinzi wa data ni muhimu. Kwa kutumia mifano fulani yako mwenyewe, Jaribu kuwafahamisha washiriki kuhusu wapi na kwa nini wao hushirikisha data zao (k.m., barua pepe za ulaghai au uhadaa) au kwa kutumia mifano iliyopo kwenye Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK-Youth).



# Somo la 3: Taarifa ya Uongo ni nini? Kwanini na kwa jinsi gani inaweza kuenea?

## Malengo ya Mafunzo

| | |
|---|---|
| Wanafunzi wataweza kutambua aina za taarifa za uongo zilizopo kwenye intaneti na kujenga ufahamu kuhusu madhara wanayoweza kuyapata. | Wanafunzi wataelewa kwanini na kwa jinsi gani taarifa ya uongo huweza kuenea kwa kasi. |

## Maswali ya tafakari yanayoweza kutumika

- ? Kwanini ni muhimu kuweza kutambua aina tofauti-tofauti za taarifa za uongo? Je, unaweza kutaja mfano wa kila aina?
- ? Je, watu unaowafahamu wameshawahi kukusambazia taarifa za uongo? Ulijibuje?
- ? Je, unaweza kutoa mfano wa kipindi uliposhirikisha taarifa ya uongo? Ulifanya nini ulipogundua kuwa taarifa uliyoshirikisha ni ya uongo?

## Changamoto zinazoweza kuibuka

**Simulizi zinazounga mkono taarifa za uongo:** Kabla ya kuangazia mada ya taarifa za uongo, pengine itakuwa vema kama utaanza kwa kutafiti aina zinazojulikana zaidi na jukwaa zinazotumika zaidi katika ushirikishaji wa taarifa hizo za uongo. Ni simulizi gani husimuliwa zaidi kuunga mkono suala la taarifa za uongo? Kujadili kweli, takwimu na vyanzo vilivyothibitishwa, kunaweza pia kusaidia.

**Washiriki washirikishao taarifa za uongo mara kwa mara:** Pengine unaweza ukapenda kutathmini kama kuna mshiriki yeyote ambaye hushirikisha taarifa za uongo mara kwa mara. Kama ndivyo, tengeneza mbinu yako binafsi ya namna ya kumlinda asije akanyanyapaliwa na kundi lililopo wakati wa kuzungumzia mada hii. Baadhi ya washiriki wanaweza wasikubaliane nae, na wakafikiri kuwa ni upumbavu kusambaza taarifa ya uongo kwa makusudi na hivyo huenda wakamnyanyasa mtu huyo. Ingawa si mbaya kupinga hoja au vitendo vifanyavyo na mtu huyu, hili halimaanishi kwamba utu au utashi wa mtu huyo unaweza kudhihakiwa.
Pia, mtu huyo asambazaye taarifa za uongo anaweza kuhisi kutishwa pindi anapofanyia kazi mada hii, jambo linaloweza kusababisha mvurugano. Jaribu kufikiria mbinu unazoweza kutumia kumjumuisha mtu huyu kwenye umoja uliopo.
Kiujumla, wahimize washiriki kuweka chachu tofauti kwa kuwa watumizi wenye ufahamu mzuri na wawajibikao vyema, wawezao kusaidia katika mapambano dhidi ya usambazaji wa taarifa za uongo, katika namna adabifu na yenye kuleta tija.

# Somo la 4: Unatambuaje taarifa ya uongo?

## Malengo ya mafunzo

| | |
|---|---|
| Wanafunzi wataweza kuchunguza usadikifu wa taarifa kwa kutumia orodha ya maswali yatakayowaongoza. | Wanafunzi wataasili kanuni msingi za uhakiki wa taarifa. |

## Maswali ya tafakari yanayoweza kutumika

- Baadhi ya mambo yaliyopo kwenye taarifa, yanayotufanya tutake kuisambaza mtandaoni, ni yapi?
- Je, unaweza kukumbuka ujumbe au chapisho la kwenye mtandao wa kijamii lililokamata shauku yako? Nini kilikufanya ufikiri kwamba ilikuwa ya kuaminika?
- Je, unaweza kukumbuka ujumbe au chapisho la kwenye mtandao wa kijamii lililokufanya ulishuku? Kama ndio, je unakumbuka namna ulivyojihisi baada ya kuliona?

## Changamoto zinazoweza kuibuka

**Wigo wa maswali ya mwongozo:** Washiriki wanaweza kuona wigo huu wa maswali ya mwongozo kuwa wa kuchosha au kulemea. Kama hili likitokea, unaweza ukawahimiza kutambua na kukariri vitu vilivyo vya umuhimu zaidi. Daima wako huru kurejea kwenye maswali haya ya mwongozo kama ikihitajika. Kuwapatia washiriki chapisho la maswali haya ya mwongozo, kunaweza kusaidia.



# Somo la 5: Taarifa ya uongo inawezaje kukuathiri na unaweza kufanya nini kuhusu hilo?

## Malengo ya mafunzo

| | |
|---|---|
| Wanafunzi wataelewa madhara yanayoweza kusababishwa na uenezi wa taarifa za uongo na kujifunza kuhusu viwango mbalimbali vya hatua za madhara yanayoweza kusababishwa. | Wanafunzi wataweza kutathmini hatua tofauti zinazoweza kuchukuliwa kuzuia uenezi wa taarifa za uongo. |

## Maswali ya tafakari yanayoweza kutumika

- Tuseme unataka kuzungumza na watu unaowafahamu kuhusu taarifa za uongo na madhara yake. Ungependa wafahamu na waelewe nini, na kwanini?
- Fikiri kuhusu viwango vya hatua za madhara zinazoweza kusababishwa na taarifa za uongo. Je, unaweza kutaja mifano mahsusi ya viwango hivi tofauti-tofauti?
- Katika Somo la 5, umejifunza kuhusu njia mbalimbali za kujibu taarifa za uongo. Ni njia zipi zinazokuvutia zaidi? Kwanini? Je, ni fanisi?

## Changamoto zinazoweza kuibuka

**Madhara na athari za taarifa za uongo:** Taarifa za uongo pamoja na athari za uenezi wake, mara nyingi huzalisha kasumba na miundo ya upendeleo na ubaguzi (tizama pia Sura ya 3). Tathmini kwa umakini mwingiliano na kiwango cha uchangamano ndani ya kundi kabla ya kujadili madhara yasababishwayo na taarifa za uongo na athari zinazoweza kutokea. Kujibu maswali yaliyoorodheshwa ndani ya Sura ya 3 kunaweza kukusaidia kutambua vichochezi vilivyopo kwenye kundi. Mwanzoni mwa vipindi vya mada hii, eleza wazi kuwa suala hili ni suala nyeti; kuzungumzia kuhusu madhara ya taarifa za uongo kunaweza kuibua hisia na mihemko mikali. Hata kunaweza kuamsha kumbukumbu za kutisha kwa baadhi ya watu. Ili kupata baadhi ya mawazo kuhusu namna ya kushughulikia hali kama hii, tizama aya iliyopo kwenye ukurasa wa 12 ihusuyo 'Uhasama wa Kidigitali na Kumbukumbu za Maumivu ya Matukio Yaliyopita.'

# Somo la 6: Hatari za ulimwengu wa kidigitali ni zipi?

## Malengo ya mafunzo

| | | |
|---|---|---|
| Wanafunzi wataweza kutambua aina tofauti za uhasama wa kidigitali katika maisha yao ya kila siku. | Wanafunzi watatambua madhara yanayosababishwa na uhasama wa kidigitali na kuelewa kwamba uhasama wa kidigitali unaweza kuenea nje ya ulimwengu wa mtandao. | Wanafunzi wataangazia namna za kuenenda kwa usahihi pindi mtu fulani, ikiwa ni pamoja na wao wenyewe, anapoathiriwa na uhasama wa kidigitali. |

## Maswali ya tafakari yanayoweza kutumika

- Taarifa za uongo, hasa hasa uenezi wake, unawezaje kuchochea uhasama wa kidigitali?
- Unafikiri tofauti kuu zilizopo baina ya uhasama wa mtandaoni na uhasama wa nje ya mtandao ni zipi?
- Uhasama wa mtandaoni na ule usio wa mtandaoni si mara zote huweza kutambulika hivyo. Kwanini hili linaweza kuwa tatizo?
- Kumbuka mfano uliokuwepo mwishoni mwa Somo la 6. Kwa namna gani ungemsaidia mtu yule aliyeathiriwa? Ungefanya nini kujilinda? Wapi ungeweza kupata usaidizi wa kuaminika na wa kitaalamu?
- Je, umewahi kujikuta katika hali iliyokufanya ujihisi kuhangaika kihisia mtandaoni? Kama ndio, ulifanyaje?

## Changamoto zinazoweza kuibuka

**Uhasama wa kidigitali na kumbukumbu za maumivu ya matukio yaliyopita:** Kuzungumzia kuhusu uhasama wa kidigitali kunaweza kuchochea kumbukumbu za hali za kufadhaisha au za kuhuzunisha. Kama hili litatokea ndani ya muktadha wa karakana, likumbushe kundi kwamba hisia kali zinaweza kuibuka wakati wa kuzungumzia mada hii na kwamba ni muhimu kuachilia hisia hizi. Kwa kuziruhusu hisia hizi kali, unaweza kutua mzigo uliokuwepo ndani ya wale walioathiriwa. Tafadhali zingatia kwamba, mtu anayeonyesha hisia zake waziwazi anaweza akadhihakiwa au kunyanyaswa licha ya maneno yako ya kumfariji. Pengine unaweza kumfuatilia mtu huyo husika ili kumjulia hali na kumsaidia. Ikiwa atakuwa hana uhakika kuhusu nini cha kufanya ili ajihisi ahueni, unaweza kumpatia mawazo kadhaa: labda huenda angependa kunywa maji, kula kipande cha pipi, kwenda kwenye matembezi na mtu, kuzungumza na mtu au kukaa kimya peke yake na kufanya mazoezi kadhaa ya upumuaji. Kisha rudi kwa kundi: je, kundi linahitaji kutumia mbinu zozote kuondoa mivutano yao, au pengine wangependelea kuzungumzia kuhusu kile kilichotokea?

Kiujumla, kuzungumzia kuhusu uhasama au mada nyingine zinazofanana na hiyo huhitaji umakini na kiwango kikubwa cha kujali katika upande wa wakufunzi. Unafanya nini kuonyesha kujijali?

Pia ni muhimu kutengeneza eneo salama ambapo kila mtu atajihisi huru (kukaribishwa), ambapo mawasiliano na miingiliano ya kistaarabu huhimizwa, na ambapo usalama wa nje umehakikishwa kadri iwezekanavyo.

Aidha, utumizi wa mifano ya kubuni unaweza kupunguza hatari za kuamsha vichochezi hivi. Mifano ya kubuni husaidia kutengeneza umbali baina ya mada na hali binafsi walizopitia washiriki husika.

**Uonevu wa kwenye mitandao ya kijamii:** Uonevu wa kwenye mitandao ya kijamii mara kwa mara huwa na madhara yasambaayo hadi nje ya mipaka ya intaneti. Huweza kwenda sambamba na miundo mingine ya uhasama kama vile unyanyasaji au uonevu. Hata hivyo, uonevu wa kwenye mitandao ya kijamii, unaweza kuvuka mbali zaidi ya suala la uonevu pekee, hivyo kuufanya kuwa mgumu zaidi kuudhibiti. Maudhui yakishaingizwa kwenye intaneti, huwa ngumu kuyaondoa. Hili linamaanisha kwamba mtu aliyeathiriwa na uonevu wa kwenye mitandao ya kijamii anaweza kukumbana na maudhui ya kudhuru tena hapo baadae – wakati mwingine miaka kadhaa baada ya kutokea kwa kisa cha awali. Hali hii hufanya uponyaji wa aina hii ya unyanyasaji kuwa mchakato mgumu sana. Katika hali nyingi, wale walioathiriwa hushindwa kukomesha hali hiyo peke yao. Kama mkufunzi, unaweza kusisitiza kwamba, kutafuta msaada si ishara ya udhaifu, na badala yake mara nyingi, hii huwa ndio namna pekee ambayo mtu huweza kutumia kutoka kwenye hali iletayo madhara.



# Somo la 7: Unawezaje kujilinda na kuwalinda wengine dhidi ya ukatili wa kidigitali?

## Malengo ya mafunzo

| | | |
|---|---|---|
| Wanafunzi wanaweza kutathmini kwa umakini athari wanayosababisha kwa familia na marafiki zao kutokana na mwenendo wao mtandaoni, k.m., wakati wa kushirikisha taarifa (za uongo). | Wanafunzi watatathmini njia na mipaka ya kushughulikia uhasama wa kidigitali, hasa unyanyasaji na uonevu wa kwenye mitandao ya kijamii. Wanapaswa kuweka usalama wao katika nafasi ya kwanza pindi wanapotathmini njia walizonazo (kujilinda kwanza kabla ya kuwalinda wengine). | Wanafunzi watafahamu namna ya kuripoti kwa siri, mienendo hatarishi iliyopo kwenye jukwaa za mitandao ya kijamii. |

## Maswali ya tafakari yanayoweza kutumika

? Uhasama wa kidigitali unaweza kusababisha sintofahamu; tunaweza tukataka kuwasaidia wengine lakini kwa kuwasaidia tukajikuta tumejiweka hatarini. Je, umewahi kupitia hali kama hii mtandaoni au nje ya mtandao? Kama ndio, nini kilikusaidia kuamua cha kufanya? Je, uliiheshimu mipaka yako mwenyewe? Kama sio, nini kingeweza kukusaidia kuamua cha kufanya? Unawezaje kuhakikisha kuwa unaheshimu mipaka yako mwenyewe?

? Je, umewahi kuripoti uwepo wa maudhui hatarishi, kama vile maoni ya kutukana au matamko ya chuki, kwa waendeshaji wa jukwaa husika au kwa watu wanaokuzunguka? Kama sio, kwanini? Kama ndio, uliripoti kwa namna gani?

## Changamoto zinazoweza kuibuka

**Kujilinda kwanza kabla ya kuwalinda wengine:** Baadhi ya vijana hufanya mambo kwa kusukumwa na hisia kali za kutaka haki itendeke. Huenda wao hujiona kuwa kama walinzi wa wale walioathiriwa kwa kutengwa na kufanyiwa uhasama. Katika vitendo vyao vya kishujaa, wanaweza kwa upesi kupoteza dira ya umuhimu wa kujilinda wenyewe. Pengine kuhimiza kwamba kujilinda mwenyewe kuna umuhimu sawa sawa na ule uliopo katika kuwalinda wengine, kunaweza kusaidia. Suala la kutoa au kutokutoa msaada kwa mtu linaweza kusababisha mgongano wa ndani au sintofahamu. Hatua ya kwanza ya kutoka nje ya sintofahamu hii ni kuheshimu uwezo na mipaka binafsi uliyonayo. Labda unaweza kufikiria mfano wa kutoa ili kufafanua sintofahamu inayoweza kutokea pamoja na hatua zinazoweza kuchukuliwa. Pengine unaweza pia kutaka kuwapatia washiriki taarifa za wapi pa kwenda kutafuta msaada endapo kama wameathiriwa na uhasama wa kidigitali. Shule zilizopo kwenye eneo lako zinaweza kuwa na washauri nasaha, ama wale walioathiriwa wanaweza kwenda hata kwa mwalimu wanayemuamini. Aidha, kuna njia ya kutafuta msaada kupitia simu za dharura zilizopo kwenye eneo lako. Kwa njia mbadala, unaweza

kumualika mtaalamu asaidiaye watu walioathiriwa na uhasama (wa kidigitali) ili azungumze kuhusu kazi yake au kutoa mafunzo ya karakana.

## Somo la 8: U tayari sasa kuyakabili mawimbi ya bahari kuu!

### Malengo ya mafunzo

| | |
|---|---|
| Wanafunzi watapitia vipengele husika vya usalama wa kidigitali kulingana na namna vinavyohusiana na wao wenyewe na watu wengine. | Wanafunzi watahisi kutiwa moyo wa kuenenda kistaarabu wanapoabiri katika Intaneti, kushiriki kwa uamilifu katika kufuma eneo la kidigitali, na kuonyesha ushupavu ndani ya eneo la kidigitali pale inapohitajika. |

### Maswali ya tafakari yanayoweza kutumika

? Kumbuka mambo uliyojifunza kutoka kwenye masomo yote. Ni nini hasa kimekusaidia wewe binafsi kuweza kuabiri kwa usalama kwenye intaneti? Kwanini? Ni nini ambacho bado kinakupa changamoto?

? Ni eneo gani mahsusi ungependa kujifunza zaidi? Unawezaje kuwa kijana Mdadisi wa Kidigitali (Digital Enquirer) mahiri zaidi?



## Unawezaje kutumia Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK-Youth) katika kuunga mkono mafunzo ya vijana?

Kama mkufunzi, unaweza kutumia Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK-Youth) katika namna mbalimbali – mtandaoni na nje ya mtandao. Mawazo machache yako hapa. Pengine wewe na wakufunzi wengine, mnaweza kufikiria njia za kufanya mawazo haya kufaa zaidi hadhira na maudhui yako uliyoyalenga?

(1) **Kutoa misaada isiyobana uhuru wa mtu, kwa ajili ya michakato ya mafunzo ya kujitegemea:** Wanafunzi vijana wanaweza kujifunza Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth) peke yao na kwa kasi yao wenyewe, ndani ya muda wao wa ziada. Unaweza kuwapatia fursa ya kuuliza maswali au kuzungumzia kuhusu namna hali yao binafsi ya kujifunza ilivyokuwa, wakiwa peke yao ama wakiwa katika midahalo ya kundi. Muundo huu wa usaidizi usiobana uhuru wa mtu, unaweza kufanyika pia kulingana na uhitaji uliopo, na bila kuwepo kwa maandalizi mengi ya maudhui husika. Hata hivyo, njia hii huhitaji uwepo wa kifaa cha simu na muunganisho mzuri wa intaneti.

(2) **Kuandaa vyumba vya mada mahsusi kwa ajili ya tafakari:** Kwa kufanya maandalizi machache, unaweza kualika vijana kujifunza somo fulani kwa kipindi fulani cha muda. Mkakati huu wa moja kwa moja unakuwezesha kujizatiti katika mada fulani. Kwa kuwa kila mtu yu na kiwango chake cha ujuzi, unaweza kuangazia mada husika katika namna fulani lengwa na kisha kuruhusu muda wa tafakari makini kufanyika baadae. Unaweza kuandaa vyumba vya tafakari katika muundo wa eneo la mtandaoni ama katika muundo wa mkutano wa ana kwa ana.

(3) **Kuendesha karakana za mada husika:** Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth) hufaa pia kwa ajili ya matumizi ya karakana zihusuzo mada za muda mrefu zaidi au katika siku za miradi ya shule. Kwa mfano, inaweza kutumika katika karakana ya kudumu masaa fulani, izungumziayo mahsusi taarifa za uongo. Unaweza kuwaalika washiriki vijana wa karakana hiyo kupitia mafunzo husika ya mtandaoni peke yao au ndani ya makundi madogo-madogo, na kisha kujadili na kutafakari kwa pamoja. Katika hali hii, mafunzo ya Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK-Youth) yanaweza kutumika badala ya maudhui mengine na kuwezesha utendaji wa midia-anuai ndani ya kipindi cha karakana.

### Vidokezo

**Upatikanaji wa vifaa vya simu:** Haijalishi muundo wako wa kipindi au karakana ukoje, kila mara hakiki kama kila mtu ana kifaa cha simu na muunganisho mzuri wa intaneti, k.m., akiwa nyumbani. Pia hakiki kama kifaa stahiki cha kiufundi kimetolewa kwenye eneo ambalo unakusudia kutumia Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK-Youth). Je, kuna vifaa vya simu vya kutosha kwa ajili ya kundi hili? Je, muunganisho wa mtandao ni mzuri na wa kasi?

**Matumizi ya midia-anuai:** Matumizi ya midia-anuai miongoni mwa vijana hutofautina. Mara nyingi hili hutegemeana na vifaa vya simu walivyonavyo na muunganisho wa intaneti walionao. Kadri vijana wanavyotumia muda mwingi zaidi mtandaoni, ndivyo kadri wanavyozoea kuabiri mandhari ya kidigitali. Tofauti zilizopo katika matumizi ya midia-anuai miongoni mwa kundi la vijana zinaweza kuleta hali ya ukosenefu wa usawa na misuguano. Ili kushughulikia ukosenefu wowote wa usawa kwa ufanisi, jaribu kupata ufahamu angavu zaidi kuhusu mwenendo wa matumizi ya midia-anuai kwa kila mwanakundi. k.m., kwa kufanya tafiti fupi.

## Ninaweza kutumia njia gani kupanua maudhui ya Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK-Youth) kwa kina zaidi?

Unaweza kupanua na kuchimba kwa kina zaidi maudhui ya Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth). Wazo la wapi pa kuanzia liko hapa. Kuwa huru kuliboresha zaidi na kutengeneza njia ya kwako mwenyewe!

### Wazo: Kitabu cha kumbukumbu cha Mtandaoni

Wawaalike washiriki kutumia kitabu cha kumbukumbu cha mtandaoni kwa kipindi cha wiki tatu. Pengine ungependa kutumia maelezo yafuatayo kulitambulisha zoezi hilo:

"Kwenye kitabu chako cha kumbukumbu cha mtandaoni, andika yale unayokutana nayo ukiwa mtandaoni, ikiwa ni pamoja na vitu unavyovifanya katika mitandao ya kijamii. Jiulize:

- Nini kinaamsha shauku yangu?
- Ninabonyeza viungo gani vya intaneti?
- Ninashirikisha jumbe au chapisho gani?
- Je, ninahakiki taarifa kabla ya kuituma?
- Nini hunifanya kushuku jambo?
- Je, kuna uwezekano kuwa nimekumbana na taarifa ya uongo au maoni ya chuki?

Andika kwenye kitabu chako cha kumbukumbu kile unachokiona."

Ikiwezekana, endesha mdahalo kila wiki kuzungumzia yale washiriki waliyoyaona. Kuanzia wiki ya pili, waulize washiriki kama wamegundua mabadiliko yoyote kwenye matumizi yao ya mitandao na kwenye mwenendo wao wa mtandaoni yaliyotokana na utumizi wao wa kitabu cha kumbukumbu cha mtandaoni.

# Sura ya 3: Tafakari juu ya unyeti wa masuala ya mgogoro, maumivu ya matukio yaliyopita, na mwingiliano wa upendeleo na ubaguzi

Tafakari maswali yafuatayo kuhusu kundi lengwa mahsusi unalotaka kufanya nalo kazi, na mazingira ya kijeografia, ya kijamii na ya kisiasa unayofanyia kazi.

## Unyeti wa Suala la Migogoro


- Je, mada ya somo lililochaguliwa, ikiwa ni pamoja na mifano na misemo iliyotumika, inaweza kusababisha mivutano ndani ya kundi?
- Je, ninafahamu nini kuhusu uwepo wa mivutano au migogoro yoyote ndani ya kundi au katika mazingira yake ya karibu? Je, suala lililosababisha mvutano au mgogoro huu lina uhusiano wowote wa karibu na maudhui ya somo la Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali kwa Kijana (DEK Youth)? Kama ndio, tengeneza mawazo mahsusi kuhusu namna ya kuzuia au kushughulikia mivutano yoyote inayoweza kuibuka baadae. Nini kinaweza kuimarisha mshikamano na hali ya kuaminiana miongoni mwa wanakundi?

## Unyeti wa maumivu ya matukio yaliyopita

- Je, ninafahamu hali zozote za sasa au zilizopita (vurugu) ambazo zimesababisha mikwaruzano na mifadhaiko mingi kwa mtu mmoja mmoja au kwa kundi?
- Je, maudhui ya somo hili, au mfano au misemo iliyotumika, inaweza kuamsha kumbukumbu za mifadhaiko ya kale kwa watu, na kusababisha hisia kali na kuibuka tena kwa mfadhaiko upya. Kama ndio, tengeneza mbinu kwa ajili yako au kwa ajili ya kundi la wakufunzi, ya namna ya kushughulikia hali zinazoweza kuwa za kichochezi. Pia, daima kumbuka kuhusu umuhimu wa kujijali.

## Mwingiliano wa upendeleo na ubaguzi

- Je, una fahamu visa vyovyote vya hivi karibuni vya ubaguzi ndani ya kundi? Kwa mfano, je, kuna memba wa kundi hili aliyeonewa kutokana na kuwa na sifa au mwonekano fulani?
- Je, kuna visa vya ubaguzi na upendeleo vilivyotokea ndani ya mazingira ya kijamii ya memba wa kundi? Kwa mfano, je, kuna baadhi ya vijana hawana zana za kutumia Intaneti? Kama ndio, hili linawezaje kuathiri mwingiliano na mshikamano wa kijamii ndani ya kundi?
- Je, kuna visa vyovyote vya upendeleo uhusianao na maudhui ya Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (DEK Youth) ndani ya kundi, unaoweza kuchochea fedheha au kujenga msingi wa ubaguzi hapo baadae?



**Makala ya Tamati**

Digital Enquirer Kit ya Vijana – Kitabu cha Mwongozo cha Wakufunzi

Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH

Agosti 2022

**Muundo:** Dagmar Nolden, Berghof Foundation Operations gGmbH. Muundo huu umefuatisha ubunifu-muundo wa shirika, uliotengenezwa na Tactical Tech kwa ajili ya Digital Enquirer Kit.

**Leseni na haki za utumizi:**

**Kitabu cha Mwongozo na DEK ya Vijana:** Kazi hii imekatiwa Leseni ya Kimataifa chini ya shirika la Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0. Kutizama nakala ya leseni hii, tembelea http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0/

**Picha:** p-didakt. Picha zote zilizo na vipengele na viumbe vya majini zinaweza kutumika katika muktadha wa mafunzo ya mtandaoni, sifa zote zikielekezwa kwa mtengenezaji wa picha hizi kwa madhumuni yasiyo ya kibiashara, kwa jina la Creative Commons Attribution-NonCommercial-NoDerivs 2.0 Germany License. Kutizama nakala ya leseni hii, tembelea http://creativecommons.org/licenses/by-nc-nd/2.0/de/ Picha zilizo na maumbile ya kibinadamu zimetolewa www.humaaans.com na https://undraw.co na CCO bure.

Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (Digital Enquirer Kit Youth) ilitengenezwa kati ya miezi ya Desemba 2021 na Agosti 2022 kwa ushirikiano baina ya Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH na Seitenstark e.V. Waandishi walikuwa Michael Schulte na Dagmar Nolden (Berghof Foundation). Mradi huu ulisimamiwa na Daniela Divjak (GIZ). Bodi makini ya wataalamu wa kimataifa, miongoni mwa wengine, iliwajumuisha Mahishaa Balraj (Hashtag Generation), Gajithira Puvanendran, Lillian Kariuki (Watoto Watch Network), Dr. Elvis Fokala (Children Rights Unit, University of Pretoria), J. Andrew Baker (ILGA World) na Kundi la Vijana Washauri la Kimataifa, lililopitia maudhui yote, lilihusika pia kwa sehemu kubwa. Chombo cha p-didakt kiliwajibika kushughulikia masuala ya kiufundi. Baadhi ya maudhui yaliyopo kwenye Nyenzo ya Mdadisi wa Kidigitali ya Vijana (Digital Enquirer Kit Youth) na  yamejumuisha maboresho mahsusi ya kundi lengwa ya Digital Enquirer Kit, ambayo yalitengenezwa na Tactical Tech kwa kushirikiana na GIZ. Mradi huu ulifadhiliwa na Wizara ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo pamoja na Tume ya Ulaya.

Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH Registered Offices: Bonn: Friedrich-Ebert-Allee 32 + 36, 53113 Bonn, T +49 228 44 60-0, F +49 228 44 60-17 66; Eschborn: Dag-Hammarskjoeld-Weg 1 – 5, 65760 Eschborn, T +49 6196 79-11 15 I E info@giz.de I www.giz.de I Registered at: Local court (Amtsgericht) Bonn: HRB 18384, Local Court (Amtsgericht) Frankfurt am Main: HRB 12394 I Chairperson of the Supervisory Board: Martin Jäger (State Secretary at the Federal Ministry of Economic Cooperation and Development) I Management Board: Ingrid-Gabriela Hoven, Thorsten Schaefer-Guembel.